

**Markscheme
Barème de notation
Esquema de calificación**

May / Mai / Mayo de 2022

Swahili / Swahili / Swahili B

**Higher level – Paper 2 – Listening comprehension
Niveau supérieur – Épreuve 2 – Compréhension orale
Nivel Superior – Prueba 2 – Comprensión auditiva**

© International Baccalaureate Organization 2022

All rights reserved. No part of this product may be reproduced in any form or by any electronic or mechanical means, including information storage and retrieval systems, without the prior written permission from the IB. Additionally, the license tied with this product prohibits use of any selected files or extracts from this product. Use by third parties, including but not limited to publishers, private teachers, tutoring or study services, preparatory schools, vendors operating curriculum mapping services or teacher resource digital platforms and app developers, whether fee-covered or not, is prohibited and is a criminal offense.

More information on how to request written permission in the form of a license can be obtained from <https://ibo.org/become-an-ib-school/ib-publishing/licensing/applying-for-a-license/>.

© Organisation du Baccalauréat International 2022

Tous droits réservés. Aucune partie de ce produit ne peut être reproduite sous quelque forme ni par quelque moyen que ce soit, électronique ou mécanique, y compris des systèmes de stockage et de récupération d'informations, sans l'autorisation écrite préalable de l'IB. De plus, la licence associée à ce produit interdit toute utilisation de tout fichier ou extrait sélectionné dans ce produit. L'utilisation par des tiers, y compris, sans toutefois s'y limiter, des éditeurs, des professeurs particuliers, des services de tutorat ou d'aide aux études, des établissements de préparation à l'enseignement supérieur, des fournisseurs de services de planification des programmes d'études, des gestionnaires de plateformes pédagogiques en ligne, et des développeurs d'applications, moyennant paiement ou non, est interdite et constitue une infraction pénale.

Pour plus d'informations sur la procédure à suivre pour obtenir une autorisation écrite sous la forme d'une licence, rendez-vous à l'adresse <https://ibo.org/become-an-ib-school/ib-publishing/licensing/applying-for-a-license/>.

© Organización del Bachillerato Internacional, 2022

Todos los derechos reservados. No se podrá reproducir ninguna parte de este producto de ninguna forma ni por ningún medio electrónico o mecánico, incluidos los sistemas de almacenamiento y recuperación de información, sin la previa autorización por escrito del IB. Además, la licencia vinculada a este producto prohíbe el uso de todo archivo o fragmento seleccionado de este producto. El uso por parte de terceros —lo que incluye, a título enunciativo, editoriales, profesores particulares, servicios de apoyo académico o ayuda para el estudio, colegios preparatorios, desarrolladores de aplicaciones y entidades que presten servicios de planificación curricular u ofrezcan recursos para docentes mediante plataformas digitales—, ya sea incluido en tasas o no, está prohibido y constituye un delito.

En este enlace encontrará más información sobre cómo solicitar una autorización por escrito en forma de licencia: <https://ibo.org/become-an-ib-school/ib-publishing/licensing/applying-for-a-license/>.

1. For questions where candidates must write their answers, do not award the mark if the answer is incomplete, or if there is additional information that is irrelevant or shifts the focus of the answer. However, accept other words with the same meaning as the correct answers in the markscheme.
2. Accept spelling and grammatical mistakes provided they do not change the meaning of the answer. For the gap-fill question type, however, the answers must fit the gaps grammatically.
3. For questions where candidates choose an answer from options, if two answers are given – one in the box and one outside – only mark the answer inside the box.
4. Words inside brackets in this markscheme are optional: candidates may include these words in their answer, but they are not essential for the mark to be awarded. If there is more than one possible answer to a question, these answers are indicated by a slash (/).
5. This markscheme must be read in conjunction with the Marking Instructions for the relevant component on IBIS.

1. En ce qui concerne les questions pour lesquelles les candidats doivent rédiger leurs réponses, n'attribuez pas le point si la réponse est incomplète, ou s'il y a des informations supplémentaires qui ne sont pas pertinentes ou qui modifient l'objet de la réponse attendue. Néanmoins, l'utilisation de mots ayant le même sens que les bonnes réponses est acceptée dans le barème de notation.
2. Les erreurs d'orthographe et de grammaire sont acceptées si elles ne changent pas le sens de la réponse. Cependant, les réponses insérées dans un texte à trous doivent être grammaticalement correctes.
3. En ce qui concerne les questions pour lesquelles les candidats doivent choisir une réponse parmi plusieurs propositions, s'ils ont donné deux réponses différentes, l'une à l'intérieur de la case et l'autre en-dehors, ne prenez en compte que la réponse qui se situe dans la case.
4. Les mots entre parenthèses dans ce barème de notation sont facultatifs : les candidats peuvent les inclure dans leur réponse, mais ils ne sont pas essentiels pour justifier l'attribution du point. S'il y a plus d'une réponse possible à une question, celles-ci sont indiquées par une barre oblique (/).
5. Ce barème de notation est à lire parallèlement aux instructions de notation disponibles sur IBIS pour la composante concernée.

1. En las preguntas en las que los alumnos deban responder por escrito, no otorgue la puntuación si la respuesta está incompleta, o si aportan detalles adicionales que cambian el enfoque o no son pertinentes. No obstante, acepte otras palabras con el mismo significado que las respuestas correctas en el esquema de calificación.
2. Acepte los errores de ortografía y gramática, siempre y cuando no modifiquen el significado de la respuesta. Sin embargo, en las preguntas de completar la oración, las respuestas deberán concordar gramaticalmente con su contexto.
3. En las preguntas en las que los alumnos deban elegir una opción, si se han escrito dos respuestas (una dentro de la casilla y la otra fuera), puntúe únicamente la que esté dentro de la casilla.
4. Las palabras entre corchetes en este esquema de calificación son opcionales: los alumnos pueden incluirlas en la respuesta, pero no son fundamentales para que se otorgue la puntuación. Si hay más de una respuesta posible a una pregunta, esto se indica con una barra (/).
5. Este esquema de calificación debe leerse junto con las instrucciones para la corrección del componente en cuestión disponibles en IBIS.

Kifungu A

Swali		Jibu lengwa	Kubali	Usikubali	Alama
1.		A			1
2.		C			1
3.		B			1
4.		C			1
5.		C			1
				Jumla	5

Kifungu B

Swali	Jibu lengwa	Kubali	Usikubali	Alama
6.	A, B, E, G, I	Kwa mpangilio wowote, alama [1] kwa kila jibu sahihi		5
7.	kuvunja mguu	aliteleza ngazini		1
8.	mezani			1
9.	chakula cha nyumbani			1
10.	furaha			1
11.	mhogo, mdalasini na limau			1
			Jumla	10

Kifungu C

Swali	Jibu lengwa	Kubali	Usikubali	Alama
12.	vyombo vya habari			1
13.	utafiti			1
14.	ubinafsi			1
15.	wazazi wangu	wazazi wake		1
16.	kukwepa macho			1
17.	A, D, E, H, J	Kwa mpangilio wowote, alama [1] kwa kila jibu sahihi		5
			Jumla	10

Kifungu A

Utasikia kipande cha podikasti ya mwandishi wa habari chipukizi akiwa katika kijiji karibu na Nairobi.

Presenter	<p>Habari gani wasikilizaji wetu. Karibuni kwenye podikasti yetu ya wiki hii ambapo tutazungumza na Wambui anayeishi maili tano nje ya Nairobi. Wambui ametualika ili tuje kujionea mgao wa kazi katika familia yake. Familia ina jumla ya watu sita.</p> <p>Kama wengi hapa kijijini, wazazi wake ni wakulima, wanaishi kwa kuitegemea ardhi, ingawa baba yake ana mifugo. Wao wanategemea zaidi kilimo cha mama yake ingawa mara nyingine huenda kuvua mtoni. Wambui na ndugu zake watatu husaidia kazi za nyumbani. Wambui anahisi fahari kubwa kuwa kifungua mimba katika familia yake ingawa hii inamaanisha kwamba yeye husaidia zaidi nyumbani huku akiwa mfano mzuri kwa ndugu zake ambao anawaongoza. Lakini kwanza, hebu tumfahamu. Wambui, tafadhali wasalimie wasikilizaji wetu.</p>
Wambui	Habari zenu nyote
Presenter	Sasa mmeshasikia sauti yake. Wambui, hebu tuambie hapa kuna changamoto gani kwako na kwa familia yako.
Wambui	<p>Sisi hatuna raha ya maji yanayotiririka au maji ya kutoka bombani. Tunatumia masaa mengi huku tukitembea umbali mrefu ili kuchota maji kwa matumizi ya kila siku. Hapa kijijini kwetu kwa kawaida ni wanawake ambao huwa na kazi ya kutembea masafa marefu ili kuteka maji. Nilikuwa nina hamu ujionee hilo lakini kwa bahati mbaya, kila kitu kimebadilika wiki hii na hali kuwa juu chini chini juu; badala ya kuwepo kwa ukame tuliuzoea kila siku, kumekuwa na mvua kubwa mno ambazo zimefanya mto ujae sana, barabara ziteleze sana na kuwa na tope na hata madaraja yamekuwa hatari.</p>
Presenter	<p>Ndiyo, nimeona hiyo nilipokuwa njiani leo. Sasa kabla ya kusikia zaidi kuhusu hali ya hapa, hebu tuisikilize nguvu ya mvua inavyonyesha.</p> <p>Sawa wasikilizaji, bila shaka mmefurahi kumsikia binti huyu. Sasa niambie Wambui, kwa nini hujaenda shule leo?</p>
Wambui	<p>Ni salama zaidi kuwa nyumbani. Kawaida leo ningekuwa mtoni, nachota maji. Mimi huchota maji asubuhi kabla ya kwenda shuleni na pia jioni wakati ninaporudi hapa kijijini. Ndugu zangu husaidia jioni tu.</p> <p>Lakini leo tumeweka ndoo na makopo uwanjani na zinajaa maji ya mvua. Pale zinapojaa tunahifadhi maji kwenye mapipa yaliyo ndani.</p>
Presenter	Kwa hivyo unaweza kusema kwamba umesalimika kutokana na safari nyingi ambazo ingebidi kuzifanya za kuenda mtoni.
Wambui	Ndiyo, sasa ninatupia macho ndoo, zinapojaa tunamimina maji kwenye mapipa ndani. Haya maji tutayatumia kwa muda mrefu. Pia, maji ya mvua ni mazuri zaidi kwani hayana chumvi chumvi kama yale ya mtoni.
Presenter	Kwa hivyo mmevuka janga la ukame na kuingia kwenye mvua kubwa.
Wambui	Ndiyo kutoka janga moja na kuingia jingine. Tunashukuru huku kwetu hakujafurika.
Presenter	Bila shaka! Asante sana Wambui kwa kuzungumza nami leo.

Kifungu B

Utasikia mwisho wa taarifa ya habari ambapo msichana anayeitwa Hannah anahojiwa kuhusu kitabu chake cha mapishi.

News anchor	Mwisho kabisa tumsikilize binti anayeitwa Hannah ambaye ameandika kitabu cha mapishi katika muda wa miezi mitatu. Karibu Hannah.
Hannah	Asante
News anchor	Hebu tuambie ilikuwaje?
Hannah	Hivi majuzi niligundua kwamba, kwa nia na madhumuni yote, sisi kama familia tulikuwa tumepoteza utamaduni wetu wa kula ambao katika jadi yetu sisi, kula ni aina ya sanaa. Ninasema hivyo kwani kitamaduni wakati wa mlo, sisi sote hukaa mduara kwenye mkeka huku tukiwacha nafasi katikati ili sinia kubwa la chakula liweze kuwekwa hapo. Kila mtu huketi kwa kukunja miguu na hula kwa mkono wa kulia, mkono wa kushoto ni utovu wa nidhamu. Matonge ya mwanzo huchukuliwa kutoka kwenye upande wa sinia ulio mkabala na mlaji. Kwa njia hii, tunaweza kujifunza tabia njema kwani hakuna mtu anayethubutu kula chakula ovyo ovyo, hata watoto pia. Mikono haigusani kamwe, kufanya hivyo ni tabia mbaya. Tunapomaliza kula, tunangojeana hadi sote tunapomaliza kula ndipo tunanawa mikono yetu kabla ya kusafisha nafasi ambayo tuliikalia. Nilipokuwa mtoto niliona kama kusaidia usafi kulikuwa kukinipotezea muda, lakini sasa sijali kwa kweli.
News anchor	Sasa mlipotezaje utamaduni huu?
Hannah	Ni kwamba tu, polepole miaka ilivyoenda, tulianza kula chakula chetu kwa nyakati tofauti. Tena hata wakati wa wikiendi ambapo sisi sote huwa pamoja nyumbani, tulikula mbele ya televisheni, kila mmoja wetu akiwa ameshika uma na kisu huku akila chakula chake bila ya kutambua kwamba tulikuwa tumeacha kujumuika pamoja. Mama yangu alilalamika kwamba kama familia, tulikuwa na tabia mbaya ya kula lakini hakuna mtu aliyemsikiliza.
News anchor	Sawa, sasa kabla hatujaendelea kusikiliza kilichotokea, hebu tuungane na familia ili tuone aina hii ya kula.

News anchor	Asante sana kwa kutushirikisha sote. Sawa, sasa Hannah hebu tuambie nini kilitokea na kuleta mabadiliko.
Hannah	Amini usiamini, mama yangu aliteleza ngazini na kuvunja mguu. Sisi kama familia tulilazimika kubadili maisha yetu na kukaa ndani ili kumsaidia. Hatukuruhusiwa kutoka nje kamwe. Niligundua kuwa kula chakula kwa pamoja kama familia ni muhimu sana na nilitoa wazo kwa wanafamilia tuanze kula angalau mlo mmoja mezani kwa pamoja, si mkekani kama tufanyavyo kimila, lakini mezani. Kila mtu alikubali na kamwe hatujaiwacha tabia hiyo.
News anchor	Kweli inavutia, lakini kwa nini hamkukaa mkekani?
Hannah	Ah ni kwa sababu meza ni rahisi zaidi kwani hatuhitaji kuitoa na kuirudisha tena na tena kama mkeka.
News anchor	Muda unatutupa mkono, hebu niambie kuhusu kitabu chako.
Hannah	Nilivutiwa na kusaidia jikoni na kuandika mapishi. Mwanzoni nilifikiri ningeweza kutumia mapishi nitakapoenda chuo kikuu ambapo ningepika chakula cha nyumbani, pia ingekuwa njia nzuri ya kujenga urafiki. Lakini nikaamua kukichapisha na sasa kimeleta furaha kwa watu wengi sana.
News anchor	Ni kweli kabisa. Je kuna siri zozote za mapishi ya familia yako?

Hannah	Ndiyo. Sisi hutumia vyakula vya kawaida sana, kwa mfano, huongezea unga wa mhogo kwenye mikate na pia tunapenda kutumia mdalasini ambao huleta harufu nzuri pia tunatumia limau kwenye karibu kila mapishi! Jaribu.
News anchor	Nitafanya hivyo. Asante Hannah kwa kujiunga nasi leo. Sasa hebu tuangalie matangazo ya hali ya hewa.

Kifungu C

Utasikia hotuba ya Juma anayezungumza kuhusu suala la vijana kujihusisha na jamii.

Announcer	Tunamkaribisha bwana Juma kwenye jukwaa letu leo ili azungumze kuhusu mada ya vijana kujihusisha na jamii. Bwana Juma, karibu.
Juma	<p>Asante sana! Ninashukuru kupata fursa hii. Nianze kwa kuwaomba mtafakari kama nyinyi mmeona kwamba vyombo vya habari huweka mkwazo mkubwa suala la vijana kuwa na ubinafsi na kuwepo haja kwao kujihusisha zaidi na ustawi wa jamii zao. Hii inahimiza na kuendeleza mtazamo kwa ujumla kwamba vijana hawashiriki au hata kujiingiza katika masuala ya kijamii. Sasa mimi nimekuwa nikijiuliza, wamefikiaje hatima hii? Na je, vijana hufikiria nini? Nilitaka kufahamu ukweli. Katika jitihada zangu, niliamua kufanya utafiti.</p> <p>Nilitambua haraka kwamba, kutokana na sababu sizioeleweka, kila kizazi huwa na mawazo kwamba vijana wa kizazi hicho wana ubinafsi mkubwa sana! Yaani watu huwaona vijana kuwa ni watu wanaojifikiria wao tu na si watu wengine wowote. Fikra za bibi na babu yangu kuhusu kizazi cha wazazi wangu ni sawa na fikra za wazazi wangu kuhusu kizazi changu mimi.</p> <p>Kwa mfano, wazazi wangu hulalamika kuhusu vijana kwenye usafiri wa umma. Wao husema kwamba ' vijana hukwepa kuangalia watu machoni kwa sababu hawataki kuwa na ustaarabu wa kuwapisha viti walivyovikalilia, hivyo hutazama chini huku wakisoma simu zao muda wote'. Wao huniambia: 'sisi tunakuambia haya ili kizazi chako kibadilike!'</p> <p>Lakini je, wanavyoona wao ndio ukweli? Mimi sidhani!</p>

Juma	<p>Kwa vile nilitaka kuhakikisha yote haya, hatua ya awali niliyoichukua ni kuchunguza kile ninachokijua kwa ubora zaidi - mitandao ya kijamii. Hii ni kwa sababu ninajua kuwa sawa na mimi, mara nyingi vijana huwa kwenye majukwaa anuwai ya kijamii. Nilizunguka humo na kuangalia akaunti za marafiki zangu na niligundua kwamba walikuwa na uhuru wa kujieleza. Wengi walijihusisha na mada tofauti ikiwa ni pamoja na zile ambazo zinaweza kuonekana za kipuuzi pamoja na pia mada nzito kama zile za uonevu. Nikajiuliza, 'inawezekana kwamba vijana hawa hujisahau wanapoperuzi simu zao na kujishughulisha na mada tofauti mtandaoni?'</p> <p>Pia kuna wale ambao ni maarufu, wanaojulikana kama washawishi muhimu mtandaoni, huwa wanawahamasisha vijana wengine na kuwashirikisha ili kutokomeza mambo hasi. Mimi ninaona kwamba huu ni mfano wa vijana kuijali jamii na tena hufanya hivyo kwa kutumia njia salama za majadiliano.</p> <p>Ninafikiri hilo ni muhimu kuliko kupisha viti kwenye basi. Hii inamaanisha kwamba vijana hujihusisha na jamii na tayari huchukua jukumu la kuwa washirika wenye dhamana. Mwisho ningesema kwamba, suala hasa la kuzungumzwa ni kwamba vijana wanahusika kwa aina tofauti; si kwamba hawajihusishi kabisa.</p> <p>Tafadhali fikirieni maneno haya. Kama mtaweza tafadhani nitumieni maoni yenu kuhusu suala hili kwa kutumia barua pepe. Asanteni kwa kunisikiliza.</p>